# Binadamu na Punda

Hapo zamani Punda na Simba waligombana. Punda hakuwa na nguvu. Alipigwa akaumia sana. Aliishi kwa woga, kwani kila alipokutana na Simba ugomvi ulianza tena.

Baada ya shida kubwa, Punda alimwomba Binadamu amsaidie. Binadamu alichukua bunduki akamwua Simba. Punda alimshukuru Binadamu, akamwambia: Asante sana. Sasa unaweza kuomba lolote na mimi nikusaidie. Binadamu akamwambia: Ninaomba unichukulie gunia langu la viazi. Gunia hilo liko kule shambani. Punda akakubali, akaenda akalibeba. Njiani Binadamu akamwambia Punda: Nimechoka sana kwa kazi niliyofanya. Nashindwa kutembea. Tafadhali nibebe. Punda akasema: Haya panda twende.

Walipofika nyumbani, Punda akamwambia binadamu kwa heri. Narudi nyumbani kwangu. Binadamu akasema: Ukirudi huko porini utapata shida. Watoto na ndugu za Simba watakuua. Kaa hapa kwangu. Punda akakubali. Tangu wakati huo, Punda akawa anafanya kazi nyumbani kwa binadamu.

**Maswali**

1. Simba na Punda walifanya nini?
2. Baada ya kuumizwa Punda alifanya nini?
3. Binadamu alitumia kitu gani kumuua Simba?
4. Gunia lilikuwa wapi?
5. Punda anaishi wapi siku hizi?

# Safari ya Mti

Hapo zamani, kulikuwa na Mti mkubwa kando ya mto. Ndege wengi walitua kwenye matawi ya Mti huo. Waliimba nyimbo na kusimuliana hadithi za vijiji vya mbali. Mti ulifurahi sana kusikiliza hadithi na nyimbo hizo. Vilevile wanyama wakija kunywa maji mtoni, walipumzika chini ya Mti huo. Walipokuwa chini ya Mti, walielezana habari za vijiji walivyotembelea.

Mti ulipata hamu ya kwenda kuona mambo yaliyosimuliwa. Lakini haukuwa na miguu wala mabawa. Haukuweza kutembea wala kuruka. Mti uliwaomba ndege na wanyama waubebe mpaka huko. Ndege na wanyama walikataa wakasema Mti ni mzito. Mti ulisikitika sana.

Mvua iliponyesha Mti ulitoa maua na kuzaa matunda mengi. Ndege na wanyama waliyala matunda hayo. Walisafiri mbali na matunda mengine. Kila walipofika walidondosha matunda ya Mti huo. Basi Mti ukaota kila mahali. Mti ukawa umesafiri kwa njia ya ajabu.

# Kibo na Mawenzi

Kibo na Mawenzi ni majirani lakini hawapendani. Zamani walikuwa marafiki. Walipendana sana, ila Kibo alikuwa mchoyo na Mawenzi alikuwa mlafi.

Siku moja Mawenzi alikwenda kwa Kibo kuomba moto. Alimkuta Kibo anasonga ugali. Ugali ulikuwa unanukia vizuri. Mawenzi aliomba moto. Akapewa, akaondoka. Alipofika njiani akauzima ule moto.

Mawenzi akarudi kwa Kibo, akakuta Kibo hajapakua chakula. Mawenzi alichukua tena moto, lakini alipofika njiani aliuzima tena. Akarudi tena kwa Kibo. Kibo alikuwa ameanza kupakua. Aliposikia hodi alifunika chakula. Akasimama na mwiko mkononi. Alijua kuwa Mawenzi anataka chakula. Hakumpa chakula wala moto. Alimpiga na mwiko kichwani na mabegani. Mawenzi alibonyea kichwani. Mawenzi naye aliinua chungu cha ugali akammwagia Kibo kichwani. Mawenzi alikimbia akarudi kwake. Hadi leo Mawenzi amebonyea bonyea kichwa. Kibo naye bado ana kofia nyeupe kama ugali mweupe kichwani.

**Maswali**

1. Mawenzi alifuata nini kwa Kibo?
2. Nani alikuwa mlafi?
3. Kibo alimpiga Mawenzi sehemu gani?
4. Nani bado ana kofia kama ugali kichwani?

# Panya na Binadamu

Hapo kale wanyama wote waliishi porini. Binadamu aliishi kijijini. Alilima shamba kubwa la mahindi. Akapata mavuno mengi, akajaza ghala yake.

Panya wakamwonea Binadamu wivu. Walifanya mkutano, wakaamua kumwibia chakula chote. Usiku Binadamu alipolala, panya wakaingia kimyakimya. Wakala mahindi usiku kucha. Asubuhi walirudi porini. Walifanya hivyo mara nyingi.

Baadaye Binadamu alijua kuwa mahindi yanaibiwa. Aliwaita wanyama wote. Akawaambia: Atakayemkamata mwizi wa mahindi, nitaishi naye.

Wanyama wote walijaribu, wakashindwa. Paka aliingia ndani ya ghala akajificha. Usiku ule aliwakamata panya wengi. Binadamu alifurahi sana, akamkaribisha Paka akae nyumbani kwake. Tangu siku hiyo Paka ni rafiki wa Binadamu.

# Mbu na Tembo

Hapo kale Mbu na Tembo waliishi pamoja. Tembo hakuwa mnene kama alivyo sasa. Mbu naye hakuwa mwembamba kama alivyo sasa. Wote wawili walikuwa na miili ya kawaida.

Siku moja Tembo alimwambia Mbu waende kuishi mwituni. Alisema mwituni kulikuwa na chakula kingi na maji mengi. Mbu alikataa akasema: Mimi nitakwenda mjini. Huko nitanyonya damu ya watu. Nitanenepa haraka.

Tembo alikwenda mwituni akaishi kwa furaha. Alinenepa sana. Mbu alikwenda mjini. Binadamu hakumpenda Mbu kwa sababu Mbu huleta homa. Mbu alipotaka kumnyonya damu, Binadamu alimfukuza. Mbu alikosa damu, hivyo alikonda sana. Mpaka sasa Mbu ni mwembamba.

**Maswali**

1. Mbu na Tembo walikuwa na miili ya namna gani?
2. Tembo alikwenda kuishi wapi?
3. Je, Mbu alikwenda kuishi wapi?
4. Je, wanadamu wanampenda mbu?

# Ndege walivyopata manyoya

Hapo kale ndege hawakuwa na manyoya isipokuwa mfalme wao Mbuni. Yeye alikuwa na manyoya mengi. Aliweza kuruka juu angani. Ndege wengine walisumbuliwa na maadui kwa kuwa hawakuweza kuruka.

Siku moja ndege wote walifanya mkutano. Walimwita mfalme wao, wakamweleza shida yao. Mbuni hakujua njia ya kuwasaidia. Aliwasikitikia na kuwaonea huruma.

Mwisho wa mkutano ndege walipata njia, wakasema: Mfalme wetu mbuni, wewe una manyoya mengi. Tunakuomba utugawie ili na sisi tuweze kuruka kama wewe.

Mbuni alikubali na kuwatolea kila mmoja manyoya machache Wote waliokuwapo walipewa Ndege walifurahi sana. Walivaa yale manyoya na mara wakaruka angani. Mbuni naye akajaribu kuruka akashindwa. Manyoya yake yalikuwa yamepungua sana.

Mbuni alipoona hawezi kuruka, alijifunza kukimbia. Baada ya siku chache akawa hodari wa kukimbia. Tangu siku hiyo Mbuni haruki tena angani. Anakimbia aridhini kama wanyama.

# Binadamu na Punda

Hapo zamani Punda na Simba waligombana. Punda hakuwa na nguvu. Alipigwa akaumia sana. Aliishi kwa woga, kwani kila alipokutana na Simba ugomvi ulianza tena.

Baada ya shida kubwa, Punda alimwomba Binadamu amsaidie. Binadamu alichukua bunduki akamwua Simba. Punda alimshukuru Binadamu, akamwambia: Asante sana. Sasa unaweza kuomba lolote na mimi nikusaidie. Binadamu akamwambia: Ninaomba unichukulie gunia langu la viazi. Gunia hilo liko kule shambani. Punda akakubali, akaenda akalibeba. Njiani Binadamu akamwambia Punda: Nimechoka sana kwa kazi niliyofanya. Nashindwa kutembea. Tafadhali nibebe. Punda akasema: Haya panda twende.

Walipofika nyumbani, Punda akamwambia binadamu kwa heri. Narudi nyumbani kwangu. Binadamu akasema: Ukirudi huko porini utapata shida. Watoto na ndugu za Simba watakuua. Kaa hapa kwangu. Punda akakubali. Tangu wakati huo, Punda akawa anafanya kazi nyumbani kwa binadamu.

**Maswali**

1. Simba na Punda walifanya nini?
2. Baada ya kuumizwa Punda alifanya nini?
3. Binadamu alitumia kitu gani kumuua Simba?
4. Gunia lilikuwa wapi?
5. Punda anaishi wapi siku hizi?

# Uongo wa Nyoka

Hapo zamani wanyama wote waliishi kwa amani. Walikutana mara kwa mara kuzungumza juu ya kazi zao.

Wanyama wote walikuwa wanakutana isipokuwa Nyoka. Nyoka aliona wivu kwa sababu hana miguu kama wanyama wengine. Kwa hiyo alieneza uongo akasema: Mkutano mwingine wanyama watauana. Pundamilia amesema atampiga Simba mateke. Ngozi ya Chui itatengenezwa kiti cha kukalia Swala. Kiboko atamvunja Twiga shingo. Nyoka alisema maneno mengi ya uongo.

Wanyama wengine waliamini maneno ya Nyoka. Simba alikasirika sana aliposikia kuwa Pundamilia atampiga mateke.

Wanyama walipokutana tena kila mmoja alikuwa na hasira. Walianza kugombana. Simba alimrukia swala akamvunja mfupa na kumtafuna. Fujo ilikuwa kubwa, wanyama wote wakawa wanapigana.

Tangu siku hiyo wanyama hawapatani tena.